**102/2**

**KISWAHILI**

# MWONGOZO.

# KIDATO CHA TATU KARATASI YA PILI.

**UFAHAMU**

(a) Lazima wakubali mabadiliko / kuwa swala la mabadiliko kuhusu jinsia haliwezi kupuuziliwa mbali (alama 2)

(b) (i) Kutukanwa
(ii) Kudharauliwa
Kunyimwa
Haki kunyimwa heshima
Kunyimwa nafasi za ajira, elimu, uongozi (zozote 3x1=alama 1)

(c) (i) Jamii inathamini sana misingi ya familia/ mume na mke wa familia inayohusika wanaushirikiano mkubwa
(ii) Kiongozi ambaye hana mke au familia au Yule ambaye mke wake hatambuliki, hutiwa mashaka na jamii hata kama kiongozi aliye na azma ya kushikilia kazi ngumu ya kuongoza umma. (alama 2)

(d) (i) Kwa sababu yatalenga mafanikio ya familia na mume
(ii) Kiongozi aliyefaulu katika usimamizi wake mara nyingi huwa na mke ambaye wanashauriana
(iii) Tunaweza kuwaona wanawake mashuhuri waliotoa uongozi ambao hadi waleo unapigiwa mfano. (3x1alama 3)

(e) (i) Kukosa urithi
(ii) Maisha ya dhiki
(iii) Kubaguliwa
(iv) Magonjwa yanayoweza kuangamiza k.v. ukimwi

(f) (i) Kushamiri-kunawiri
(ii) Hadiriki- hafai/ hastahili
(iii) Azma- Nia/ kusudi

**MUKHTASARI**


Swali (a)

i. Binadamu hupenda kujivika vilemba vingi kama vile kutukuzwa na kuheshimiwa, kuombwa ushauri na kutambuliwa
ii. Wengi hukataa kufanya jambo la halali kwa kuhofia kuiwa wajinga/ wanapokosa huona ugumu wa kuomba radhi/ samahani kwa sababu ataonekana mjinga
iii. Mara nyingi mkurugenzi huita mkutano na kutisha kuadhibu watakaochelewa na mwisho yeye mwenyewe akachelewa
iv. Huwa haombi msamaha (bali) hulaumu usingizi au gari
v. Aghalabu tunapowakuza watoto, tunawafunza maadili mema/ tunawafunza umuhimu wa kuomba radhi wanapokosea wakubwa
vi. Kukosea ni kwa binadamu wote (na) huweza kuwa kwa makusudi au bahati mbaya
vii. Tunapofanya makosa ni lazima tuombe msamaha ili kuondoa kero (1x7)

**<u>Swali (b)</u>**

(i) Waja wengi huogopa kusimama mbele za watu na kuwasilisha/ kutenda jambo fulani
(ii) Huwa hataki kukosea/ hajiamini/ huenda watu wakaona kasoro yake
(iii) Hawajui kuwa kukosa njia ndiko kuijua
(iv) Wanaweza kujadili maswala ibuka na pengine huyaungi mkono maoni ya wengine kwa sababu ya imani/maadili
(v) (nawe) hutaki kutoa msimamo ingawa dhamiri yako imekwazika na baadaye hulaumu wengine ilhali ulikataa kusimama na kutetea msimamo wako.

(vi) Wengi hujichukuwa watu muhimu sana na huona mkutano/sherehe hauwezi kufaulu ikiwa hawako/hutaka watambuliwe/majina yao yatajwe
(vii) Tusiwe watu wanaotaka kutajwa au wanaolalamika ikiwa hatukuhusishwa kwenye jambo
(viii) Unaposhuhudia jambo, usiogope kutoa usaidizi au ushahidi (1x zozote 7)




Jumla = 15

**Makosa**

1. Ondoa makosa ya sarufi hadi alama 5 (makosa 10 x ½ alama)
2. Ondoa makosa ya hijai hadi alama 3 (makosa 6 x ½ alama)
(makosa ya sarufi yaadhibiwe yanapotokea mara ya kwanza tu; kwa kila aina ya kosa la sarufi, addhibu makosa mawili tofauti)

**MATUMIZI YA LUGHA**

a) /f/ - konsonanti hafifu/sghuna (al.1)
/v/ - konsonanti ghuna
b) Binadamu hawezi kumuumba mwenzake (alama 1)
(akipata kitahiniwa bila kutunga sentensi – al.½)
c) Mtoto mwenye hasira/ghadabu hawezi kuelewa maagizo (al.1)
d) Yule mshukiwa aliyekamatwa na polisi alisema, "papa hapa ndipo nilipoficha huo mkufu."
"papa hapa ndipo nilipoficha huo mkufu," Yule mshukiwa aliyekamatwa na polisi alisema. (al.3)
e) Pinde zizi hizi ndizo zilizonunuliwa jana jioni. (al.2)
(sentensi iwe na mantiki na ihusishe sehemu zote)
f) i) Ndegwa alimpa mwanafunzi kalamu yake. (al.1)
ii) Siku hizi mahitaji yamezidi na pesa hazitoshi (al.1)
**g) Rudi:** (i) Njoo tena/rejea (al.1)
(ii) Rekebisha tabia/kanya/adhibu/adilisha- hasa motto (al.1)
h) Mtume! Asimame, nusura aingie kwenye shimo la taka (al.2)
**i) – refu** : urefu (al.1)
**j) Chagizo : juu kwa juu na upepo mkali (al.1)**
k) Isije ikawa – sawa na 'isitokee kuwa' k.m. isije ikawa yeye ndiye alitenda kitendo hicho. (al.2)
(sentensi sahihi, asibadilishe kiunganishi)
l) Mwanafunzi afanikiwaye√ maishani ni Yule asomaye√ kwa bidii na pia awatiiye √ wazazi wake
('O' tamati ½ x 3 + ½ ya sentensi = al.2) (bila 'O' ya tamati asipate)
m) Anikumbukaye a-, -ni- (viambishi awali );√ -a-, -ye- (viambishi tamati) √
a- Kiambishi cha nafsi ya tatu, umoja (mtenda) √

-ni- kiambishi cha nafsi ya kwanza umoja (mtendwa)√

-a- kiishio√

-ye- kirejeshi√

n) Kijizi hakikuiba kijikapu na kigombe/kijigombe (al.2)
(swali lizingatiwe kwa ujumla, akikosa kutahiniwa chochote – 0)
o) Ukwato wa mnyama hunifaidi (al.1)
p) Mawimbi hayo ya maji yaliwahofisha wavuvi wakashindwa kutupa nyavu zao majini (al.4)
q) Sabina amesumbuliwa na kuku hawa kwa muda mrefu (al.2)
r) Sahili : sentensi yoyote sahihi yenye kitenzi kikuu kimoja/wazo moja kuu. (al.1)
Ambatani : sentensi sahili mbili zilizounganishwa (al.1)

s) S ——— KN + KT√
KN——— N + S√

N ———— Mwanasiasa√
S ———— Aliyewapuuza wanaeneo lake√
KT———— T
T ———— amekomelewa. (al. ½ x 6 =3) (sita kutuza anapokosea, asipopata mwanzo-sifuri)

t) Maimuna alimkaribisha Bakari na kumuomba/sihi akae (naye) Bakari akamshukuru na kumuuliza/kutaka kujua habari za nyumbani. (al.2)

u) Mgeni – yambwa tendewa (al.1)

**Makosa**

1) Hijai 6 x ½ = 3h
2) Sarufi makosa yote

*mwanafunzi asiadhibiwe makosa ya sarufi zaidi ya nusu ya alama alizopata katika kila kisehemu.

**ISIMUJAMII**

a) Nadharia :

i) Kiswahili kama lugha ya mseto/mchanganyiko wa lugha tofauti za kigeni na za dkiafrika. Ni zao la kuingiliana kwa lugha za kigeni kama kihindi, kiarbu, kiajemi na lugha za makabila ya wenyeji
ii) Kiswahili kama tokeo la ndoa baina ya wanawake wa pwani ya afrika mashariki na waarabu/lugha ya vizalia wa ndoa kama hio.
iii) Kiswahili ni lugha ya kibantu kulingana na ushahidi wa kiisimu na kihistoria (alama 1 x 3 =3)

b) Sifa za kimsingi za sajili ya darasani :

i. Lugha sanifu
ii. Mwingiliano wa kisarufi hudumishwa
iii. Msamiati huegemea kwenye mada husika/maneno ya taaluma mbalimbali hutumika
iv. Urudiaji/takriri – ili kuhakikisha kuwa hoja imeeleweka
v. Majibizano – kati ya mwalimu na wanafunzi wanapouliza na kujibu maswali
vi. Sentensi huweza kuwa fupi/ndefu kutegemea mada husika
vii. Imejaa ufafanuzi – wahusika wanapoelezea hoja ili ieleweke vyema

(mtahiniwa atoe maelezo au mifano, akitaja hoja tu – al 1)

(zozote 4 za kwanza x 2 =8)

**Makosa**

1) Hijai 6 x ½ = 3h
2) Sarufi 6 x ½ =3s